Swahili
Kiswahili

# Mwongozo kwa wanafunzi wanaofanya mitihani ya maandishi ya 2021 VCE

Unapaswa kusoma habari inayofuata pamoja na ushauri kuhusu mitihani ya maandishi ya VCE uliomo katika 2021 VCE Exams Navigator. Tafadhali zingatia sana kwa sehemu zinazohusu Vifaa vilivyokubaliwa kwa tathmini za nje za VCE, kanuni za VCAA, ratiba ya mitihani ya 2021 VCE na Utoaji Maalum.

*Wakati habari hii inalengwa kwa wanafunzi, inatolewa pia kuhakikisha familia/walezi wanafahamu taratibu ambazo zitakuwepo kuhakikisha tathmini zinafanywa katika mazingira ya usalama wa COVID (COVIDSafe).*

Ingawa mitihani ya maandishi ya VCE ina jukumu muhimu katika kusababisha matokeo ya mwisho kwa VCE, ikiwa hauwezi kufanya yoyote ya mitihani yako ya maandishi ya VCE kutokana na COVID-19 (UVIKO-19), utaweza kuomba kwa Hesabu Inayotokana Mtihani (Derived Examination Score) (DES).

DES imehesabiwa kwa kutumia tathmini zako za wastani zilizofanyiwa shuleni, tathmini zozote zingine za nje katika masomo, matokeo yako ya Mtihani ya Mafanikio ya Jumla (General Achievement Test) (GAT), na anuwai ya data ziada zinazotolewa na shule yako.

VCAA ina michakato iliyowekwa ili kuhakikisha unapata matokeo ya haki na ya kuaminika.

Unapaswa kuhakikisha shule yako imetoa kwako na zifuatazo:

- nakala ya **Ratiba ya Mtihani/Tathmini ya Mwanafunzi** yako ya kibinafsi inayoorodhesha tarehe, saa na mahali kwa kila mojawapo ya mitihani yako, pamoja na tarehe za mwisho za kuweka ombi la DES kwa kila mtihani na; na inapohusu
- nakala ya **karatasi ya Ushauri wa Mipangilio Maalum ya Mtihani** yako kwa mtihani wowote ambapo VCAA imekubali kwa Mipangilio Maalum ya Mitihani.

## Je, ni hatua zipi zitakuwepo ili kufanya mitihani ya maandishi ya VCE iwe COVIDSafe?

Mitihani ya maandishi ya VCE itatokea kwenye shule yako au mahali pengine kama kushauriwa na mtoaji wako wa elimu. Shule zote za Victoria na watoa wengine wakuu wa sekondari wanahitajika kuwa na Mpango wa COVIDSafe uliowekwa.

Njia anuwai za usalama zinazokubaliwa na Idara ya Afya (Department of Health) zitakuwepo kuhakikisha mazingira ya mitihani ni COVIDSafe kwa ustawi wa wanafunzi wote, waangalizi na wafanyakazi wote wa shule. Hatua hizi za usalama ni pamoja na:

- mchakato wa kusajili wakati wa kufika;
- kupanga vizuri ukumbi kwa njia inayosaidia mahitaji ya kuweka umbali wa mwili, kudumuisha mahitaji ya wiani ya mwanafunzi mmoja kwa mita za mraba 4; na
- kuweka dawa ya kuua viini kwenye madawati na viti kabla na baada ya kila mtihani, pamoja na nyuso zingine zenye kugusa sana kila mara siku nzima.

© VCAA

## Nahitaji kufanya nini kuwa COVIDSafe?

**Unapaswa**

- Kuvaa barakoa ya uso inayofunika pua na mdomo wako, kulingana na mwongozo wa sasa kwa shule za Victoria, isipokuwa uwe na msamaha kwa sababu ya ulemavu au hali ya afya. Unapaswa kuvaa barakoa yako ya uso kwa wakati wote, ikiwa ni pamoja na wakati unapofika, wakati wa mtihani, na unapotoka.
- Kufanya usafi wa mikono kila mara, pamoja na kuingia, na kutoka, ukumbi; na
- Kufanya umbali wa mwili, kuweka angalau mita 1.5 mbali na watu wengine wakati wote.

## Napaswa kufanya nini kama nina ulemavu, ugonjwa au hali nyingine zinazosababisha mimi kuwa kwenye hatari kwa kupata COVID-19?

Ikiwa una ulemavu, ugonjwa au hali nyingine inayofanya una uwezekano zaidi kuwa mgonjwa sana na COVID-19, unapaswa kuzungumza Mipangalio Maalum ya Mitihani yoyote na shule yako. Hiyo inaweza kukuruhusu kukaa m(i)tihani wako wa maandishi peke yako kwenye majengo ya shule pamoja na udhibiti wa kufaa wa kiafya na wa salama.

## Napaswa kufanya nini ikiwa naumwa katika wiki ile, au kwa siku ile ya mtihani?

**Lazima usihudhurie** mtihani ikiwa hujisikii vizuri au una dalili zozote za COVID-19, hata kama ni ndogo, pamoja na:

- kupoteza au badiliko katika harufu au ladha;
- homa, jasho la baridi au jasho;
- kikohozi, kuuma koo au kamasi yanayotoka;
- upungufu wa pumzi; na
- katika hali fulani kichwa kuumwa, uchungu wa misuli, kichefuchefu, kutapika na kuharisha pia kunaweza kuzingatiwa kuwa dalili.

Wasiliana na shule yako kwa ushauri zaidi ikiwa una dalili hizi zozote. Enda kupimwa kwa COVID-19 haraka iwezekanavyo na kaa nyumbani wakati unangoja kwa majibu yake. Julishe kituo cha vipimo au mkusanyaji kwamba wewe ni mwanfunzi wa VCE, kwani wanafunzi wa VCE wamepewa kipaumbele cha mchakato wa kipimo kuwezesha wakati wa matokeo ya haraka sana inayowezekana.

Lazima ukae nyumbani ikiwa unangoja kwa majibu ya kipimo cha **dalili za** COVID-19

Ikiwa unaonyesha dalili zozote za COVID-19 wakati wa kufika, au unakuwa kuumwa wakati wa mtihani, utaombewa kungoja kwenye eneo tofauti na mzazi au mlezi wako atapigwa simu kuja kukusindikiza.

## Ikiwa unajisikia mgonjwa na dalili za COVID-19 katika siku ya mtihani, lazima usihudhurie mtihani wako.

Unapaswa kupimwa na kukaa nyumbani mpaka unapopokea majibu yako. Ikiwa huwezi kuhudhuria mtihani, utastahili kuomba kwa DES.

Kwa kuhudhuria mtihani wa maandishi wa VCE, unahakikisha kuwa huna COVID-19 na huna dalili zozote zinazofanana na COVID-19.

## Chini ya hali gani nyingine nisihudhurie mtihani?

Kwa kuongezea ya kujisikia mgonjwa kwa siku ile ya mtihani, **lazima usihudhurie** mtihani wa maandishi ikiwa umepimwa mbaya chanya kwa COVID-19 au kama unasubiri majibu ya kipimo cha **dalili za** COVID-19. Katika hali hizi, utastahiki kuomba kwa DES.

## Vipi ikiwa nimetambulishwa kama Mawasiliano ya Karibu ya Kwanza (Primary Close Contact) (PCC)?

Idara ya Afya (Department of Health) imehakikisha kwamba wanafunzi ambao wametambulishwa kama Mawasiliano ya Karibu ya Kwanza (Primary Close Contact) wataweza kufanya mitahani yao katika chumba maalum kwa shule yao.

Ikiwa wewe umetambulishwa kama Mawasiliano ya Karibu ya Kwanza (Primary Close Contact), utahitaji kufuata maelekezo ya Idara ya Afya (Department of Health) na shule yako atawasiliana nawe kuhakikisha unaelewa mipangilio unayopaswa kufuata, ikiwemo:

- mahitaji ya karantini na kupima kwa COVID-19 iwapo kuchanjwa kamili au bado kuchanjwa kamili; na
- mahitaji ya usafiri na afya na usalama kwa kila siku ambayo una mitihani ya maandishi.

## Je, nahitaji ushahidi gani ili kuomba kwa DES kusababishwa na COVID-19?

Utastahili kuomba kwa DES kama unazuia kumaliza mtihani au kama utendaji wako umeathiriwa sana kwa sababu ya COVID-19.

Mahitaji ya ushahidi ni pamoja na:

- barua ya kuunga mkono/ ripoti ya tukio kutoka shule; na
- ushahidi wa kupimwa kwa COVID-19 – kama cheti cha kimatibabu kutoka mtaalamu huru wa afya kinachopendekeza kipimo.

## Kufungwa kwa shule kutokana na COVID-19

Ikiwa shule yako imefungwa kwa muda kutokana na COVID-19 na matokeo ya hiyo ni mtihani mmoja au zaidi hauwezi kutokea, shule yako itashughulikia na VCAA kuhakikisha hutakuwa katika hali ngumu. Hautahitaji kuomba kwa DES kama hiyo inatokea.

## Kuna msaada gani wa kiakili na wa ustawi kwa mimi?

Unaweza kupata hisia za dhiki na wasiwasi wa jumla zinaweza kuhisiwa na wewe na familia yako wakati wa kipindi cha tathmini ya nje ya VCE. Baadhi yenu mnaweza kupata motisha kutoka kwa hisia hizi, lakini wengine wanaweza kuhitaji msaada ziada kutoka familia, marafiki, mwalimu mwaminifu au mtaalamu wa kimatibabu au wa afya ya kiakili.

Ikiwa umewahi kushughulika na mtaalamu wa kimatibabu au wa afya ya kiakili zamani, sasa labda inaweza kuwa wakati mzuri kwa “kumwona” kukumbusha mbinu ili kusimamisha vizuri wasiwasi wowote ambao wewe, familia yako, marafiki au shule yako wanaweza kuwa nao.

Kuna misaada anuwai kwa wewe, kama vile:

- Seti ya vifaa vya Afya ya Akili (education.vic.gov.au)
- https://www.education.vic.gov.au/Documents/school/teachers/health/mentalhealth/quick-guide-to-student-mental-health-and-wellbeing-resources.pdf

## Ninawezaje kufanya nyingine kukaa salama kabla ya tathmini yangu?

Watu wote wa Victoria wa umri wa miaka 12 na zaidi kwa sasa wanastahiki kupokea chanjo ya COVID-19. Kupata chanjo ni njia bora ya kujilinda wewe, familia yako na jamii yetu ya shule kutoka milipuko zaidi na kuenea kwa COVID-19.

Kuchanjwa sio lazima kwa mitihani, lakini inashauriwa sana isipokuwa ambapo mtaalamu wa matibabu anakushauri tofauti. Tafadhali ongea na daktari yako ikiwa una maswali yoyote juu ya chanjo na hali yako mwenyewe wa afya.

Wanafunzi wote wanatiwa moyo kupanga kupata dozi ya kwanza kabla mtihani wao. Inapendekeza usipate chanjo yako ya kwanza kwa siku ile ya mtihani, au kwa jana yake ya mtihani – ili kuepuka kujisikia madhara ya kawaida ila ya madogo kama vile uchovu, kichwa kuumwa, maumivu ya misuli, homa na baridi na/au maumivu ya kiungo wakati wa mtihani.

Kwa maelezo zaidi, tembelea tovuti ya Idara ya Afya: Habari za Chanjo kwa watoto na vijana | Coronavirus Victoria. Hii inajumuisha maelezo yaliyotafsiriwa: Habari zilizotafsiriwa kuhusu chanjo za COVID-19 | Coronavirus Victoria.

Unahimizwa kuwa salama ya COVID-Safe iwezekanavyo katika siku na wiki inakaribia mitihani yako ya maandishi, kuepuka kuhatarishwa na COVID-19. Hii ni pamoja na kuepuka maeneo ya umma yenye watu wengi, mahali penye shughuli nyingi, au usafiri wa umma ikiwezekana.

## Nyenzo gani zinapatikana kwa wazazi/walezi?

Inaweza kuwa vigumu wakati wengine kwa wazazi kujua jinsi ya kutoa msaada mzuri sana kwa watoto wao. Nyenzo kwa wazazi na walezi ni pamoja na:

- Ushauri kwa wazazi kusaidia afya na ustawi wa mtoto wao.
- Mfuatano wa Podcast ya Kulea Wanaojifunza.

## Naweza kupata habari zaidi wapi?

Kwa ushauri zaidi wa afya, unaweza kuwasiliana  na simu ya haraka ya masaa-24 ya COVID-19 kwa 1800 675 398, GP yako au angalia tovuti ya Idara ya Afya (Department of Health): https://www.dhhs.vic.gov.au/victorian-public-coronavirus-disease-covid-19#what-are-the-symptoms-of-coronavirus-covid-19.

© VCAA